# MAHUSIANO 101:

*Namna ya Kumbaini mtu wa Kuanza Naye Mahusiano Yatakayokupeleka Kwenye Ndoa Ya Kiungu.*

**(Muhubiri 1:1-7)**

Pastor James & Frida Kalekwa

© Haki ya nakala 2018

James & Frida Kalekwa

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kutoa nakala sehemu yoyote ya kitabu kwa namna yoyote bila ruhusa ya mmiliki wa kitabu hiki isipokuwa nukuu zilizoruhusiwa kisheria.

Kimetolewa na:
Kingdom Impact Publishers (KIP)
P.O Box 1074
Mwanza, Tanzania
kingdomimpactpublishers@gmail.com
kalekwajames@gmail.com
+255-754-917-764
+255-714-762-669
**ISBN: 978-9987-9869-9-6**

Toleo la kwanza 2018-03-18

# Orodha ya Yaliyomo:

Utangulizi ........ 5

Sura ya Kwanza: Nyakati na Mazingira Pekee ambayo Mungu aliwapatia watu wenzi ........ 9

I. Adamu – mwanadamu na mwanaume wa kwanza duniani (Rejea: Mwanzo 1&2) ........ 10

II. Hosea – Nabii na Mume wa Kahaba ........ 11

III. Yusufu na Mariamu – wenyeji wa mpango wa Mungu wa Ukombozi. (Rejea Mathayo 1&2) ........ 13

Sura ya Pili: Kigezo cha Mvuto ........ 17

- Adamu alivutiwa na Hawa ........ 18
- Yakobo alivutiwa na Raheli ........ 19

Hitimisho ........ 21

Angalizo Muhimu ........ 21

Sura ya Tatu: Kigezo cha Jina ........ 23

I. Jina la kupewa na wazazi/walezi ........ 24

a) *Misingi ya kimapokeo/tamaduni (Traditional naming)-* ........ 25

b) *Sababu za ki-hali/mazingira (situational naming)* ........ 25

c) *Misingi ya ki-hatima (Prophetic naming)* ........ 25

Muhimu: ........ 26

II. Jina la kujipatia unapoishi duniani ....................26
Muhimu ..............................................................27
Geuza sarafu ........................................................28
Sura ya Nne: Ushauri binafsi kwa Kijana .................33
Kuhusu Mwandishi wa Kitabu: ................................39

# Utangulizi

Neno la Mungu liko wazi ya kwamba ni nia ya Mungu kuwasaidia watu wake na zaidi kusaidia watu wake kwenye maisha yao ya siku kwa siku. Ndivyo inavyoonekana kwenye kitabu cha Mwanzo na baadaye kwenye Mahusiano baina ya Mungu na taifa la Israeli. Hata hivyo kwasababu ya mioyo migumu na yenye ukaidi, Mungu anasema kwenye neno lake Hosea 4:6 – ukosefu wa maarifa ndiyo umekuwa chanzo cha uangamivu kwa wanadamu. Lakini Mungu ameachilia maarifa ili kumsaidia kila anayehitaji msaada na mwongozo wa Mungu kwenye maswala mbalimbali ya kimaisha (Mithali 11:9/Yohana 8:32).

Moja ya maeneo ambayo yamewachanganya vijana wengi ni namna ya kuanzisha mahusiano, kuyalea na kuyafikisha kwenye kilele cha mahusiano –NDOA. Hii ni kwasababu ya kutojua kweli ya neno la Mungu linasemaje kuhusiana na jambo hili. Hii ni kutokana na kutolipa neno la Mungu uzito stahiki kwenye maisha na badala yake kuielekea namna ya dunia hii ili kupata mwongozo. Kwa muda mwingi niliohudumia vijana mashuleni na vyuoni, vijana wengi hutafuta hekima za kisaikolojia, elimu ya malezi na nyinginezo; na wengine hutazama watu

maarufu “celebrities” kama waigizaji, wanamitindo, wanamuziki n.k kama mwongozo wa maisha ya kimahusiano.

Kuna wengine katika bidii ya kuutafuta ukweli wamejikuta wakiangukia kwenye mikono isiyo salama kwa kusikiliza nadharia (theories), hadithi za kizee (myths), mapokea (traditions), mapokeo kutokea shuhuda za watu binafsi (Watu binafsi siyo standard, NENO la Mungu ndiyo standard)… haya yameleta mkanganyiko na hali ya kuvunjwa moyo kwenye mioyo ya vijana.

Nikiwa na umri wa miaka kumi na tano (15) kwenye makambi ya vijana nimesikia mafundisho juu ya urafiki, uchumba hadi ndoa ambayo yaliibua maswali mengi moyoni mwangu kuliko majibu. Shauku kubwa iliinuka ndani ya moyo wangu na nilitafuta maarifa kiasi cha kukutana na kila aina ya fundisho. Ashukuriwe Yesu aliyenikutanisha na kitabu kidogo cha Mwalimu Christopher na Diana Mwakasege **“Mambo 12 Ya Kutafakari Kabla Kufanya Uamuzi wa Kuoa au Kuoelewa.”** Kitabu hicho kiliweka msingi thabiti sana ndani ya moyo wangu.

Baada ya kuendelea mbele na kujifunza, kupata mashauri na kusaidiwa na watumishi kadhaa wa Mungu. Leo mimi na mke wangu tunao ujasiri wa

kusema, hatujutii hata kidogo juu ya muda tuliowekeza kuitafuta kweli.

Baada ya wazazi wetu wa kiroho na wachungaji wetu, baba Goodluck na mama Ziada Kyara kutuita na kutujulisha ya kwamba wanasikia maongozi ya Mungu ndani yao ya kwamba tunapaswa kushika zamu ya kuanzisha na kuwa walezi wa huduma ya vijana ya kanisa la New Vine; walitupatia muda wa kutafakari na kumsikiliza Bwana. Baada ya siku kadhaa tulipata mpenyo wa kimungu ndani yetu na moja ya vitu ambavyo Roho Mtakatifu aliweka kwa uzito mioyoni mwetu ni kujenga msingi thabiti kwenye mioyo ya vijana kwenye eneo hili. Roho Mtakatifu alitusisitiza kufundisha kweli na si vitisho, mapokeo na desturi. Kweli itawaweka vijana huru.

Huo ndiyo moyo hasa nyuma ya uandishi wa mafundisho haya.

Tumekuombea kwa Mungu, Roho Mtakatifu ya kwamba usomapo kitabu hiki akili yako ipokee uhuru na usiishi chini ya kongwa la utumwa tena. Zaidi ya yote uchukuapo hatua, ziwe ni hatua zinazoongozwa na kweli ya neno la Mungu.

Pastor James & Frida Kalekwa<br>Huduma ya Vijana ya New Vine<br>Mwanza, Tanzania

# Sura ya Kwanza:

# Nyakati na Mazingira Pekee ambayo Mungu aliwapatia watu wenzi

Mpaka muda ambao tunaandika masomo haya, utafiti tulioufanya kwenye neno la Mungu, Biblia, unaonyesha ya kwamba kuna watu watatu tu ambao Mungu aliwapatia wenzi kwa kuwaletea moja kwa moja, ana kwa ana na kisha "*kuwalazimisha*" kukaa kwenye mahusiano hayo. Ukifuatilia kwa ukaribu utagundua ya kwamba Mungu alifanya hivyo kulingana na nyakati na mazingira na/au kwasababu ya ajenda maalum ambayo watu hao kibinafsi walibeba au mahusiano yao.

Hebu ambatana nasi kwenye kutazama mazingira na nyakati ambazo Mungu aliwapatia watu wenzi wao wa kimaisha kisha tulinganishe na mazingia yetu (yako binafsi) iwapo unaona kuna uhalali wa namna yoyote wa Mungu kukuletea mwenzi na "*kukulazimisha*" kudumu kwenye mahusiano hayo.

## I. Adamu – mwanadamu na mwanaume wa kwanza duniani (Rejea: Mwanzo 1&2)

Kwenye habari ya uumbaji, utagundua ya kwamba kila baada ya kuumba jambo fulani Mungu alifanya tathmini na kuona ya kwamba ni jema kisha siku ikakamilika. Lakini baada ya kumuumba mwanadamu- mwanamume, Adamu, Mungu aliona ya kwamba *"Si vyema…"* (Mwanzo 2:18) kuna upungufu. Mungu akafanya majaribio mawili ya kumuondolea upweke Adamu; Mosi, alifanyiza wanyama na kuwaleta mbele ya Adamu – lakini hakuonekana msaidizi wa kufanana naye (Mwanzo 2:19-20). Pili, Mungu akamlaza usingizi mzito Adamu na kutokea hapo akamtengenezea mwanadamu mwenzake, ambaye Adamu alimpa jina la mwanamke. (Mwanzo 2:21-24).

Kwenye mazingira haya Adamu hakuwa na nafasi ya kuchagua kwasababu hakuwa na machaguo ya kufanya kwa upande wa mwanadamu wa kike. Hakukuwa na mwanamke mwingine duniani… zaidi ya wanyama majike!

Kwa msingi wa andiko hili na mazingira haya ni kosa kwa kijana kudhani ya kwamba Mungu atakuletea mwenzi wa maisha yako ukiwa umelala tu mahali fulani – hapa ninamaanisha umetulia na hujishughulishi na swala la mahusiano ukidhani

Mungu anakutafutia binti/kijana wa kiume na atamshika mkono kumleta kando yako. Kijana (wa kiume na wa kike), usisahau ya kwamba wewe si Adamu!- mazingira na nyakati ni tofauti. Hakuna uhalali wowote wa kimaandiko kudhani ya kwamba namna ya Adamu itafanya kazi kwako. Hii ni kwasababu tayari umezungukwa na vijana wenzako mamia kwa maelfu, kila mahali. Mungu amekwisha maliza uumbaji. Jukumu lako ni kuchagua kutoka kwenye machaguo ambayo Mungu ameyatengeneza tayari.

Kama ambavyo kijana unavyoamini ya kwamba siku hizi Mungu huwa hatengenezi matunda wala miti ya matunda au hatengenezi mahindi au mimea yake kwasababu alipotengeneza mmea aliuwekea ndani yake mbegu na uwezo wa kuzalisha mmea husika (Rejea Mwanzo 1:12) ndivyo ambavyo Mungu huwa haumbi wanyama wapya bali kuna mbegu na uwezo ndani yao ya kuzaliana. Iwapo unaona hayo ni sawa kabisa, kipi kinakufanya udhani ya kwamba Mungu bado huwa anaumba wanawake kutokea kwenye mbavu za wanaume na kuwavizia wanaume wakiwa usingizini kisha anaweka binti kando yao?

## II. Hosea – Nabii na Mume wa Kahaba

Moja ya wito wa kinabii ambao huwa ninaushangaa sana ni huu wa nabii Hosea. Kila nabii kuna namna

yake ameitwa kulingana na nyakati, mazingira na ujumbe aliobeba. Mungu alimwita Hosea ili ayatumie maisha yake kuwa *"ubao wa kufundishia"*. Chochote ambacho Mungu alitaka kufundisha kwa taifa la Israeli (watu wake/taifa lake) alikifunua kupitia maisha ya kawaida ya siku kwa siku ya nabii Hosea. Kwasababu ya ujumbe wa kinabii aliobeba ambao ungeakisiwa kwenye maisha yake ya siku kwa siku hivyo basi Mungu aliratibu mpaka maisha ya ndoa ya Hosea kwa kumchagulia mke kwa vigezo vya Mungu na kuhakikisha Hosea anamuoa. Mungu anamuelekeza Hosea kujipatia *mrembo* kahaba – mke wa uzinzi aitwaye Gomeri.

Baadaye, huko mbeleni kwenye maisha, Mungu anayatumia maisha ya Hosea kuonyesha huzuni yake kwa taifa la Israeli alilolipenda na kulithamini kama mwanamke lakini taifa hilo linamwacha Mungu na kwenda kuabudu sanamu na miungu ya kuchonga kama vile, Gomeri mke wa nabii Hosea anavyopendwa lakini humtoroka mumewe na kwenda kulala na wanaume wengine.

Wito wa Hosea ulikuwa ni wito kweli. Kijana unayesoma kitabu hiki, hebu jiulize… Je, una wito wa Hosea? Najua jibu la haraka ni HAPANA kwasababu ya hiyo habari ya mwenzi kahaba… Swali langu hasa limelenga kukufikirisha je, una wito wa Hosea kiasi

cha kustahili kutafutiwa mwenzi maalum kabisa na Mungu? Yaani Mungu akutafutie na akulazimishe uoane naye? Ni kweli Hosea asingemuoa Gomeri unabii usingerandana, lakini wewe unadhani una "special prophetic mission" kiasi cha kuhitaji uratibu wa kimungu kiasi hicho?

Ninatambua kabisa ya kwamba ni kweli umebeba kusudi la kiungu ndani yako, lakini wewe si Hosea. Kwahiyo usikae ukisubiri tu Mungu akutafutie mwenzi huko "mitaani" kisha akutokee kama nabii Hosea kukupa wasifu wa mwenzi. Ukweli ni kwamba ukituliza akili yako vizuri, utagundua umezungukwa na machaguo mengi tu – Mungu amekuletea!

## III. Yusufu na Mariamu – wenyeji wa mpango wa Mungu wa Ukombozi. (Rejea Mathayo 1&2)

Mahusiano mengine ambayo yanaanzishwa na wanadamu husika lakini baadaye Mungu anayalizimishia ya kwamba yaendelee kuwepo hata wakati muhusika mmoja aliona ya kwamba hawezi tena kuendelea kwenye aina hiyo ya Mahusiano. Haya ni Mahusiano baina ya Yusufu na Mariamu.

Baada ya Yusufu kumposa Mariamu na huku wakiwa hawajakaribiana/hawajakutana kimwili (Mathayo

1:18) binti alionekana ana mimba kwa uweza wa Roho Mtakatifu. Mbingu zilihusika kuratibu ujauzito wa Mariamu ili kumzaa Yesu. Malaika anatumwa kupeleka ujumbe wenye taarifa maalum juu ya ujuzito huo. (**Rejea Luka 1:26-39**). Baada ya Mariamu kukubaliana na ajenda ya mbingu, bila kumshirikisha Yusufu, hii ilikuwa ni hatari kwasababu ingepelekea kuharibu mahusiano yake ambayo kimsingi yalikuwa yamefika mahala pakubwa kiutaratibu. Biblia inamweleza Yusufu ya kwamba alikuwa mtu wa haki na hivyo alikusudia kumwacha kwa siri (bila kumtangaza). (**Rejea Mathayo 1:19**). vyovyote vile, Mariamu angeishia kupata aibu ama ya kuachwa, kuoneakana ana mimba bila kukutana na mwanamume kimwili na aibu hiyo ingekuwa ni aibu kwa familia na jamaa zake. Kwa utamaduni wa kiyahudi, Mariamu angeachwa na Yusufu alistahili kupigwa mawe mpaka kifo kwa kosa la uzinzi kwasababu kidhibiti alikuwa nacho –ujauzito! Sasa fikiria ingekuwaje Mariamu anapigwa mawe ili auawe na Yesu akiwa tumboni!

Ni katika Misingi hiyo, ndipo Mungu ilibidi aingilie kati ili kuhakikisha Yusufu na Mariamu wanaendelea kuwa kwenye mahusiano yao ili kwamba mpango wa Mungu wa ukombozi utimilike na kufanikiwa (**Rejea Mathayo 1:20-25**). Isingekuwa sawa kwa Mungu kumuingiza Mariamu kwenye aibu kubwa kiasi kile

na kumuacha afedheheke, lakini pia kwa Yusufu ingekuwa ni fedheha ya kwamba anabaki na mke ambaye anajua fika ana ujauzito wa mwanaume mwingine.

Kijana, unadhani umebeba ajenda maalum sana ya kiukombozi kiasi kwamba Mungu anapaswa kuingilia kati mahusiano na kulazimisha uwe mwenzi wa kijana fulani? Hebu nikutazamishe kitu ambacho kitakushitua kiasi. Ni hivi, Mahusiano baina ya Yusufu na Mariamu yalikuwa yamekwishaanza tayari na walikuwa kwenye taratibu za kitamaduni za utoaji wa posa kabla Mungu hajaingiza ajenda ya kuzaliwa Yesu. Malaika alipotumwa kuwasilisha ujumbe wa kuzaliwa Yesu kwenye tumbo la Mariamu, hakutumwa kwenda kusema ya kwamba Mahusiano hayo si sahihi au hayafai kuwa kibebeo cha mkombozi wa ulimwengu! Ujumbe wa malaika haukuelekezwa katika kukosoa, kuchambua au hata kuvunja mahusiano yaliyoanzishwa. Bali, Mungu alionyesha kuyaheshimu mahusiano ambayo yameanzishwa na wanadamu kama walivyoridhiana wao wenyewe, kwa kuyapatia zawadi ya kupitishia Mkombozi wa ulimwengu na zaidi ya yote kuyalazimisha yasivunjike kwakuwa Mungu tayari alikuwa mdau wa mahusiano hayo.

Rafiki, Mungu anayaheshimu maamuzi yako ya kuanzisha mahusiano maadamu yatakuwa kwenye Misingi (Yusufu alimposa Mariamu – alifuata taratibu za jamii yao na alikuwa hajakutana naye kimwili) na kwasababu hiyo Mungu anaweza kabisa kupitisha ajenda ya Ufalme wake kwenye mahusiano yaliyoanzishwa kwa maamuzi ya wanadamu.

Je, unadhani uko kwenye mazingira, nyakati au una wito au ajenda maalum kama Adamu na mkewe; Hosea na Gomeri kahaba au Yusufu na Mariamu? Kama jibu ni ndiyo, basi mngojee Bwana kwa juhudi. Kama jibu ni la, usiwe na shaka. Habari njema ni kwamba, neno la Mungu linayo maelekezo kwaajili yako. Ambatana nasi kwenye sura zinazofuata ili tukuonyeshe namna unavyoweza kumbaini mtu ambaye unahitaji kuanza naye mahusiano yatakayokupeleka kwenye ndoa ya kiungu.

# Sura ya Pili:

# Kigezo cha Mvuto

Kitabu chetu kikuu cha rejea kwenye mfululizo huu ni Wimbo ulio Bora. Ni kitabu kilichoandikwa kwa mtindo wa ushairi, kama ilivyo kwa kitabu cha Ayubu, Zaburi, Mithali na Muhubiri. Kama ilivyo kwa kitabu cha Ayubu, Wimbo Ulio Bora kipo katika mfumo wa mazungumzo baina ya mwanaume mfalme (Sulemani) na mwamke mkulima (Mshulami).

Kwenye sura hii, tunakutazamisha namna ambavyo mvuto/kuvutiwa na kijana wa jinsia nyingine ni jambo sawa na muhimu. Uvutiwapo si hitimisho ya kwamba huyu ndiye au la, bali ni namna ya kukusogeza karibu kutaka kufahamu kuhusu kijana huyo miongoni mwa kundi kubwa la vijana. Tumekuombea kwa Roho Mtakatifu ya kwamba wakati unasoma sura hii, fikra zako zitafunguka kuelewa na hutaona *"watu kama miti wakienda"*.

Mvuto ni jambo la kiungu na jambo linalokuita ili utazame kitu cha ndani zaidi. Kila utamaduni na nyakati huwa na namna yake ya kuwasilisha hisia.

Kwenye tamaduni za mashariki ya kati, busu si jambo la ajabu, aibu au ni miiko (taboo). Kama ilivyokusalimia kwa kupiga magoti kwenye baadhi ya tamaduni za kiafrika.

**Wimbo Ulio Bora 1:2-3a**

***"Kubusu na anibusu kwa kinywa chake. Maana pambaja zako zapita divai; Manukato yako yanukia vizuri"***

Kabla hatujachukua hatua kubwa sana kutafakari, kuna neno "pambaja" linajitokeza kwenye huo mstari maana yake ni upendo (Ukisoma lugha ya kiingereza utaona neno "Love").

Kwenye mstari huu mwanamke mshulami anawasilisha ni kwa namna gani anavutiwa na mfalme. Huu si mvuto wa kiroho. Anavutiwa na midomo na manukato yake.

- **Adamu alivutiwa na Hawa (Rejea Mwanzo 2:18-25) –** Mungu alipopitisha gwaride la wanyama mbele ya Adamu ili kuona huenda kutokea kwa hao angepatikana msaidizi wa kufanana naye. Adamu aliwapatia majina na kuwaacha waende zao. Lakini, alipotoka kwenye usingizi na kukuta kiumbe cha

namna nyingine, Adamu alivutiwa na akaonyesha hisia *(hisia ni vionjo vya ndani vya mtu/ ni mwitikio wa ndani wa mtu kulielekea jambo fulani – viko kwenye nafsi na muumbaji wa hisia ni Mungu).* Ni kweli hakuwa na machaguo ya wanawake kadhaa lakini alijua kuna tofauti kati ya mwanamke na wanyama waliowasilishwa mbele yake na Mungu. Ndiyo maana mistari inayofuata inaonyesha mwitikio wa Adamu baada ya kumuona mwanamke.

**Mwanzo 2:23-24**

***"Adamu akasema, Sasa huyu ni mfupa katika mifupa yangu, na nyama katika nyama yangu, basi ataitwa mwanamke, kwa kuwa ametwaliwa katika mwanamume. Kwa hiyo mwanamume atamwacha baba yake na mama yake naye ataambatana na mkewe, nao watakuwa mwili mmoja."***

- **Yakobo alivutiwa na Raheli (Rejea: Mwanzo 29:17-20)**

***"Naye Lea macho yake yalikuwa dhaifu, lakini Raheli alikuwa mzuri wa umbo, na mzuri uso. Yakobo akampenda Raheli akasema,***

***Nitakutumikia miaka saba kwa kumpata Raheli, binti yako mdogo…”***

Unaona nini kwenye mistari hii? Yakobo alifanya ulinganifu baina ya Lea na Raheli, kwa kutumia vigezo vyake vya uzuri ama vitu anavyovutiwa na navyo, alihitimisha ya kwamba Raheli ni mzuri wa **umbo** na **uso**. Hili umbo na uso vinavyotajwa hapa si umbo la kiroho wa si uso wa kiroho – *usijaribu kurohosha!*

Ni muhimu ukajua ya kwamba uzuri wa umbo na uso ni kwa mujibu wa aonaye huo uzuri. Kuna msemo husema, *“uzuri wa kitu, u machoni pa mtu atazamaye.”* Ni “*subjective*”. Kwa hiyo basi, Lea ni mwanamke mzuri sana wa umbo na uso pindi atakapokutana na mtu anayevutiwa naye. Na Raheli ameonekana ni mzuri kwa Yakobo na si mwanaume mwingine.

## Hitimisho

Mvuto ni matokeo ya utendaji wa kimaajabu wa Mungu katika uumbaji wake – ni Bwana asifiwe kabisa! Amewaumba watu wengine kuwa warefu, wafupi, wembamba, wanene, weusi, weupe- kuna kila aina ya uumbaji wa Mungu ambao unawasilisha uzuri **Rejea Zaburi 139:13-14**, *"Nimeumbwa kwa namna ya* ***ajabu*** *na ya* ***kushangaza****."* Kijana, vile ulivyo wewe ni mzuri kwa kuwa aliyekuunga tumboni mwa mama yako ni Mungu mwenyewe.

Kwa sababu hiyo, hakuna kitu kama madai ya kwamba Mungu amekuongoza kuanza Mahusiano yanayokupeleka kwenye ndoa na binti Y au na kijana wa kiume X lakini hauvutiwi naye lakini Roho Mtakatifu anakulazimisha!

## Angalizo Muhimu

Mvuto siyo mwamuzi wa mwisho katika kuyaanza mahusiano bali ni mwito kwako kutazama kwa kina kuna nini ndani ya boksi. Katikati ya vijana wengi (wa kike na wa kiume) mvuto ndiyo hukusogeza kwa kijana mwenzako mmoja ili umfahamu zaidi kabla ya kufaanya maamuzi na kuchukua hatua moja mbele.

Kumbuka neno la Mungu lina jambo la kusema kuhusu kuutegemea mvuto kama kigezo pekee cha

kufanya maamuzi ya kuhusiana na kuanza mahusiano.

**Mithali 6:25,**
**“Usiutamani uzuri wake moyoni mwako; Wala usikubali akunase kwa kope za macho yake.”**

**Mithali 31:30,**
**“Upendeleo hudanganya, na uzuri ni ubatili; Bali mwanamke amchaye BWANA , ndiye atakayesifiwa.”**

# Sura ya Tatu:

# Kigezo cha Jina

Kama tulivyokudokeza awali kwenye sura iliyotangulia ya kwamba, mvuto ni *mwito* kwako na si kigezo cha mwisho. Baada ya kuvutiwa unapaswa kwenda kwenye hatua inayofuata. Hebu tutazame kitabu chetu cha mwongozo hapa:

**Wimbo Ulio Bora 1:3,**
***"Manukato yako yanukia vizuri; Jina lako ni kama marhamu iliyomiminwa; kwahiyo wanawali hukupenda."***

Mwanamke mshulami alivutwa na mwonekano wa mfalme lakini hakuishia hapo. Hatua inayofuata ni kutazama jina. Anasema, "*… jina lako ni kama marhamu iliyomiminwa…*" Marhamu ni aina ya manukato. Utakubaliana nasi ya kwamba manukato husambaza harufu yake pale yanapomiminwa au yanapotolewa kwenye chombo chake cha kuhifadhia. Hii ndiyo kusema, binti huyu anasikia harufu njema ya jina la kijana huyu wa kiume. Na ni kwasababu ya harufu ya jina binti mshulami anasema, "… *kwahiyo*

*wanawali hukupenda."* Wanawali, ni mabinti walioandaliwa tayari kwaajili ya kuolewa. Kama ilivyokuwa miongo kadhaa kwenye tamaduni za baadhi ya makabila ya kitanzania ya kwamba binti anapofikisha umri fulani, jukumu kubwa linalomfuata mbele yake ni kuolewa. Hivyo binti hupelekwa kwenye mafunzo maalum kama vile *kuchezwa, unyago n.k*

Kwa kutumia kigezo cha jina – harufu njema ya jina, mabinti walio tayari kuolewa "*waliofundwa*" wanampenda kijana huyu.

Hebu tukudondolee kidogo juu ya upaji wa majina. Kuna namna mbili kubwa ambazo mtu hujipatia jina

I. **Jina la kupewa na wazazi/walezi** –Mara nyingi majina haya hutolewa wakati wa kuzaliwa. Kuna mazingira ambayo hupelekea watu kubadili majina ukubwani (Rejea Danieli 1:6-7). Kwa ujumla wake, majina haya hutolewa kwa Misingi hii:

a) ***Misingi ya kimapokeo/tamaduni (Traditional naming)***- Kila jamii ina utaratibu wake wa kuiongoza. Kuna jamii ambazo hutoa majina kwa kurejelea majina ya mababu, mabibi au watu kwenye ukoo. Lengo lao hasa huwa ni kutunza majina yao yasipotee juu ya uso wa nchi.

b) ***Sababu za ki-hali/mazingira (situational naming)-*** Jina hutolewa kulingana na nyakati, mazingira au tukio ambamo mimba ilitungwa, mtoto alizaliwa au nyakati ambazo wazazi walipitia mpaka kumpata mtoto husika. (1 Nyakati 4:9-10/Kutoka 2:10/1 Sam 1:20&27).

c) ***Misingi ya ki-hatima (Prophetic naming)*** – Ama kwa kuongozwa na Mungu, au kwa ushuhuda wa ndani ya moyo (conviction) au kwa sababu ya nia njema ya mzazi/mlezi juu ya mtoto. Jina hutolewa kwa kumaanisha kule aendako mtoto husika kimaisha (hatima). Jina huakisi hatima. (Rejea Mathayo 1:21)

**Muhimu:**

Nia yetu kuambatanisha dondoo ya utoaji wa majina hapa, si kusema ipi ni mbaya au nzuri. Tumekusudia kuonyesha namna watu wanavyopata majina.

II. **Jina la kujipatia unapoishi duniani** – Kuna majina ambayo mtu hujitengenezea mwenyewe kwa tabia, mwenendo na maisha ya siku kwa siku. Watu wanaokuzunguka au wanakutana na wewe mara kwa mara hukupa jina kulingana na vile unavyojiwasilisha mbele yao. Mifano ya majina ambayo watu walijitwalia kwa maisha yao kwenye Biblia iko mingi, baadhi ni hii: **Masikini** Lazaro (Japokuwa jina Lazaro maana yake ni Mungu ndiye tegemeo langu), Rahabu **yule kahaba** (Japokuwa aliingia kwenye Orodha ya mashujaa wa imani kwenye kitabu cha Waebrania lakini bado anarejelewa kama kahaba), Iskanda – **mfua shaba**, Nabali – mpumbavu kama lilivyo jina lake, Daudi – **mtu aupendezaye moyo wa Mungu** (ingawa alitenda makosa mengi tu wakati wa uhai wake), Yuda Iskariote (Pamoja na kwamba alikuwa ni mwanafunzi wa Yesu na kuna wanafunzi walifanya makosa mengi tu lakini

huyu ni ishara ya makosa/usaliti) , **Bikira** Mariamu (Japokuwa baada ya kumzaa Yesu alizaa ndugu zake Yesu na kwahiyo si bikira tena lakini hurejelewa hivyo). Bartimayo **kipofu** (Huyu hata jina lake halisi halitajwi na maandiko kwasababu ***bar*** ni "mwana wa" kwa lugha ya Kiebrania ni kama ilivyo "bin" kwa lugha ya kiarabu... Huyu ni mwana wa Timayo -Kipofu).

**Muhimu**

Ni jambo la msingi sana kufahamu kijana, ya kwamba kila jina linapotamkwa au kutajwa, kuna sifa fulani huambatana na hilo jina – huwa linatoa harufu fulani. Kwahiyo, baada ya kuvutiwa na kijana (wa kike au wa kiume) fulani, usiishie hapoa wekeza muda kufahamu jina lake. Jiulize je jina la ninayetaka kujenga mahusiano naye linatoa harufu gani? Je, jina lake ni mithili ya marhamu iliyomiminwa kiasi kwamba wanawali humpenda? Au jina lake likitajwa hakuna mtu yuko radhi kutakwa kuambatanishwa na jina hilo?

**Geuza sarafu**

Kila sarafu ila pande mbili pacha. Kuichagua sarafu ni kuchagua pande zote mbile. Kuibeba sarafu ni kuzibeba pande mbili pacha za sarafu. Na ndivyo yalivyo maswala ya kuanzisha Mahusiano. Baada ya kutumia kila vipimo ujuavyo kuwapembua vijana wenzako na kuwaweka kwenye mizania: Kipimo cha uzuri wenye mvuto kwako na hatimaye kipimo cha harufu inayotolewa na jina. Ni hekima iwapo utajua tangu awali ya kwamba hata wewe unapembuliwa na kupimwa. Je, unao ujasiri wa kumwambia kijana anayevutiwa na wewe ya kwamba wewe ni mzuri na una jina jema na kumthibitishia hivyo? Je, uko radhi kumuhakikishia ya kwamba hatajuta ya kwamba alikuchagua wewe? Hebu tazama asemacho binti mshulani:

**Wimbo Ulio Bora1:5-6,**

***"Mimi ni mweusi-mweusi, lakini ninao uzuri, Enyi binti za Yerusalemu, mfano wa hema na za Kedari, Kama mapazia yake Sulemani. Msinichunguze kwa kuwa ni mweusi-mweusi, Kwasababu jua limeniunguza. Wana wa mamangu walinikasirikia, Waliniweka niwe mlinzi wa mashamba ya mizabibu; Bali shamba langu mwenyewe sikulilinda"***

- Mwanamke mshulami anao ujasiri na nafsi yake. Inawezekana kwenye zama zake kulikuwa na viwango (standards) ambavyo vilitumika kuamua uzuri wa binti. Maandiko yanaashiria ya kwamba rangi ya ngozi kilikuwa ni kipimo kimojawapo. Japokuwa anapungua kwenye kiwango hicho cha uzuri lakini bado anakaza kusema, ***"... lakini ninao uzuri..."*** Ana uhakika na vile alivyo. Kijana unaweza kujiwasilisha hivyo mbele ya kijana mwenzango ambaye umepembua hapo awali? Binti huyu anakaza ya kwamba rangi ya ngozi yake si asili (si ya kuzaliwa nayo) bali ni matokeo ya kuchapa kazi!

- Anaita umakini kwenye uzuri wa ndani zaidi. Kwenye mistari tuliyotangulia kunukuu hapo kabla, utaona ya kwamba kuna uzuri ambao huyu binti anajivunia na anautumia kuwanyamazisha mabinti wengine ***"...enyi binti za Yerusalemu...",*** na wanawali ***"...kwa hiyo wanawali hukupenda..."*** (Rejea Mstari 3) ambao walikuwa wanamkodolea macho kijana anayempenda. Mabinti hao wanamzidi kwa rangi ya ngozi lakini yeye anajipambanua

kama mwanamke anayefanya kazi kwa bidii kiasi kwamba amepoteza uzuri wa ngozi yake, ***"…waliniweka niwe mlinzi wa mashamba ya mizabibu…"***.

Swali letu kubwa hapa ni kwamba, Je, iwapo aina ya kijana unayemtafuta ili kuanzisha naye mahuasiano atakuwa kwenye harakati za kutafuta, unadhani atakupata wewe? Je, baada ya kumpembua kijana unayevutiwa naye kwa kutazama uzuri wake ambao unakuvuta kutazama jina lake, unao ujasiri wa kuwasilisha sifa zako na kujitaja ya kwamba wewe ni mtu sahihi na hatajuta kuwa na wewe? – Una thamani yoyote ya kuwasilisha mbele zake?

**Unawezaje kutambua tabia ya mtu?**

**Wimbo Ulio Bora 1: 5-6 – Kwenye mistari hii utaona haya:**

*a)* Kiwango chake cha utii, heshima na adabu – *"wana wa mama yake (kaka zake na dada zake) walimshurutisha kulinda mashamba, na kwa hekima anaona ni vyema afanye hivyo kazi badala ya kubishana au kufanya fujo."*

b) Kufanya kazi –*"aliwekwa kuwa mlinzi wa mashamba (siyo shamba moja) ya mizabibu."*

c) Kuwazia mambo ya watu wengine (Kuna tofauti kati ya kujidharau na kujali) – *"anamimina nguvu na akili zake kulinda mashamba ya mizabibu ya ndugu zake kiasi cha kukosa muda wa kulinda "shamba lake"*

d) Tabia yake hasa kwenye nyakati za changamoto/anapokuwa pressed – Yakobo 1:2

- Tabia ya mtu hudhihirishwa wakati anapojaribiwa
- Namna gani anashughulika na migogoro, hasira na katika hali ya kutokukubaliana na jambo fulani/pale anapokuwa na mawazo tofauti na wengine?
- Je, yuko radhi kusamehe?

# Sura ya Nne:

# Ushauri binafsi kwa Kijana

Kwa kuwa mwanadamu ni roho yenye nafsi iishiyo ndani ya mwili hivyo basi ndoa na mahusiano yatakayokupeleka huko ni swala la kiroho, kinafsi na kimwili. Ni swala la **kiroho** ndiyo maana tunawekeza muda kusoma maelekezo ya Mungu kwenye neno lake na kutafuta msaada wa Mungu kwa njia ya maombi; Ni swala la **kinafsi**- mahala penye utashi, akili na maamuzi kwahiyo mambo yanapaswa kuwekwa kwenye mizania na kupimwa, kuchambuliwa na kisha kufanya maamuzi kama vile ufanyavyo maamuzi mengine. Na ni jambo la **kimwili** na kwasababu hiyo lazima kuweko na mvuto, kupenda na kufurahia vile alivyo kijana (wa kiume au wa kike).

Tumeona ni hekima tuambatanishe "*checklist*" ya kukusaidia kufanya maamuzi kwa kuwa mahusiano ni swala linalomuhusisha mwanadamu katika ukamilifu wake (holistic).

- ***Neno la Mungu*** *(Yoshua 1:8; Zaburi 1:2-3; Zaburi 119:105)* – Neno la Mungu ndiyo

kipimo cha juu cha maisha ya mwamini (higher standard of living) na mwamuzi wa mwisho (supreme) juu ya swala la mahusiano. Kwahiyo, baada ya kuguswa na mvuto na kulifahamu jina la kijana fulani. Hebu wekeza tena muda kutulia kwenye neno la Mungu. Usiende kwa mihemko, kufuata mkumbo wala kwa ushabiki. Unapaswa kuongozwa na neno la Mungu. Habari njema ni kwamba neno la Mungu haliko kimya – limeshazungumza juu ya hayo yote. Sikiliza kijana, shuhuda za watu hata kama unawaheshimu na wamefanikiwa kiasi gani, ni nzuri lakini si mwamuzi wa mwisho. Neno la Mungu ndiyo kipimo.

- ***Amani ya Kristo ndani ya moyo*** (*Wakolosai 3:15)* – Mungu huyaongoza maisha ya mwanadamu kwenye eneo la maamuzi kwa kutumia amani ya Kristo ndani ya moyo. Hii ni mfano wa taa za kuongozea magari barabarani "Traffic Lights" ambazo husema "simama", au "nenda", au "kaa tayari". Kuna taa ndani yako. Iwapo unaelekea kufanya maamuzi yasiyo sahihi huwa moyo wako unachefuka, kama kuna dhoruba au mawimbi ya bahari. Unakosa utulivu na

raha kabisa. Kuna hali ya majuto au huzuni inafunika moyo wako. Wakati mwingine ni huzuni ambayo hukupelekea kuchoka au hata kusinzia (Unakumbuka wanafunzi wa Yesu? Walilala kwasababu ya ile huzuni). Kama unaelekea kwenye maamuzi sahihi utasikia hali ya wepesi kwenye moyo wako. Usijaribu kupuuza hata kama mvuto na jina viko sawa.

- ***Maongozi ya Roho Mtakatifu*** *(Yohana 16:13)* – Roho Mtakatifu humwongoza mwamini kwa utulivu na utaratibu. Halazimishi wala hapigi makelele. Kwahiyo, kuna nyakati utasikia sauti kama inakunong'oneza, inakusihi au inakubembeleza kiasi kwamba ni rahisi kuipuuza. ***Tahadhari:*** *Kama huwa hauna mahusiano na Roho Mtakatifu na hutafuti maongozi yake kwenye mambo madogo na mambo ya kila siku, tafadhali usijaribishie kwenye swala la mahusiano.*
- ***Mashauri ya watu wakubwa na waliokutangulia kwenye eneo husika*** *(Mithali4:1-2; 1:8; 2:1-5; 5:1)* – Ni vizuri ukatambua ya kwamba wewe si wa kwanza kuingia kwenye mahusiano. Na ya kwamba Mahusiano si jambo jipya kabisa duniani.

Kuna watu wamekutangulia kwenye njia hiyo na kwa neema ya Mungu wanaendelea kujifunza na kufanikiwa. Ninakushauri ujipatie mtu/watu (wanandoa) wacha Mungu, wakomavu (Biblia huwataja kama wazee), wanaodhihirisha mfano kwenye maisha yao na utafute kwao mashauri, hekima na shuhuda kutoka kwenyeuzoefu wa maisha ili usipigane vita ambayo ungeishinda kwa kujifunza kwa waliokutangulia.

- ***Mashauri ya watu wengine*** *(Mithali 15:22; 20:18; 24:6)* – Hapa uwe na mduara wako wa ndani ambao mnasimama nao kwenye maswala ya kimsingi ya maisha (Kama Meshaki, Shadraka, Abednego na Danieli). Hapa sizungumzii genge la "*washakaji*" au "*mashosti*". Ni watu wa rika ambao huwa mnawajibishana kwenye maswala ya maisha.
- ***Tumia akili kupima na kuchambua*** *(Wafilipi 4:8; 1 Pet 4:7)* – Ni mara ngapi Roho Mtakatifu huwa anakuambia uchane nywele? Upige mswaki? Mambo mengi ambayo umeshajua kweli zake Mungu hukuacha utumie akili kwa kuwa unaijua njia ya kuiendea kwa msaada wa kweli.

Akili iliyozoezwa kufanya mapenzi ya Mungu hufikia maamuzi sahihi. Izoeze akili yako kutenda sawasawa na kweli ya neno la Mungu. Kama neno limeshasema, usisubiri kutokewa kwenye ndoto. Neno la Mungu limesema tusitumaini akili, haimaanishi tusitumie!

- ***Fanya maamuzi*** *(Yoeli 3:14).* Neno litasema, Amani ya Kristo itakuongoza, utapokea mashauri lakini hatimaye **wewe** ndiye unayepaswa kufanya maamuzi! Baada ya yote unapaswa kuchukua hatua ya kimaamuzi.

Pia, tunakushauri usome matoleo yote matatu ya masomo haya kwani yamelenga kuwa tofali juu ya tofali jingine katika kumjenga kijana wenye mguso chanya.

Karibu uabudu nasi katika ibada za kanisa la New Vine kwa ratiba ifuatayo:

JUMAPILI
Saa 3:00 Asubuhi – 6:30 Mchana

ALHAMISI
Saa 11:00 Jioni – 12:30 Jioni

Ratiba za fellowship ya huduma ya vijana ni kwa ratiba ifuatayo:

Kila Ijumaa ya pili ya mwezi

Muda: Saa 10:30 Jioni – 12:30 Jioni

Ibada zote hizi zimeandaliwa kukupeleka mbele katika kila eneo la maisha yako.

**Mawasiliano:**

Mchungaji Kiongozi:
Pastor Goodluck & Ziada Kyara:
+255-754-435-951/+255-756-544-483

Mchungaji wa Vijana:
Pastor James & Frida Kalekwa
+255-754-917-764/+255-714-762-669

Facebook/Instagram: New Vine Youth Ministry

**Kuhusu Mwandishi wa Kitabu:**

James Kalekwa ni mume wa mke mmoja aitwaye Frida Kalekwa na baba wa watoto watatu (Joshua-Vision, Charis "Tai" na Victor). Ni mchungaji, mwandishi na mwanataaluma. Ameandika jumla ya vitabu 3 vinavyoshikika (1. Wokovu ni Uhakika wa Maisha ya Sasa na ya Baadaye, 2. Kanuni zitendazo kazi ndani ya Ufalme wa Mungu Hapa Duniani na 3. Iandike Njozi.

Amekuwa mwanataaluma wa ngazi ya ukufunzi katika Idara ya Sosholojia, Kitivo cha Sayansi ya Kijamii na Mawasiliano kwenye Chuo Kikuu cha Mt. Augustino (Mwanza) kwa muda wa miaka 3 mfululizo (2012-2015). Kwa sasa huwasilisha mada na kuchangia mijadala kwenye majukwaa mbalimbali ya kitaaluma. James ni mshauri mwelekezi (consultant) wa Ustawi kitaasisi (Organizational Development), mwanamikakati (strategist) na muwezeshaji kwenye maeneo hayo. Ameshauri taasisi na harakati mbalimbali za kijamii, kitaaluma na kiimani na kuwasaidia katika uundaji wa nyaraka za kimikakakti (strategic documents).

Pamoja na mambo mengine mengi, Kwa miaka mitano mfululizo sasa James na mke wake mzuri hufanya kazi ya kichungaji chini ya kanisa la New Vine Church (NVC) kama mlezi wa huduma ya watoto na sasa ni hulea huduma ya vijana, na mchungaji shiriki (associate pastor). Pia hufanya kazi na kampeni ya *Unashamed Lives* katika nafasi ya Msimamizi wa Upandaji wa Makanisa na

Mkurugenzi wa Mawasiliano (Church Planting Administrator and Communication Director) – Ambayo imepanda jumla ya makanisa 14 kisiwa cha Kome, 8 kisiwa cha Maisome na 15 mji wa Bunda mpaka sasa.

Kwa miaka mitano (5), amefanya kazi za kujitolea za kijamii zinazohusisha vijana na watoto. Pia ameshiriki katika kuibua, kuandika na kutekeleza miradi mbalimbali ya kijamii ndani na nje ya nchi kwenye taasisi mbalimbali kama vile *Youth of United Nations Association (YUNA)* na taasisi mama ya *United Nationa Association of Tanzania (UNA)* ngazi ya mkoa wa Mwanza na Kanda ya Ziwa, Best Buddies Tanzania (BBT) – nchini Tanzania na *Kolvi Toimintta* – yenye mradi wa kuwezesha vijana wa kiume wakimbizi – jijini Tampere, nchini Finland. Kwa misingi hiyo amejikusanyia utajiri wa ujuzi, maarifa na uzoefu wa jamii na uhalisia wake.

Shauku ya moyo wake ni ***kuujaza ulimwengu kwa maarifa ya utukufu wa Mungu kama maji yaifunikavyo bahari. (Habakuki 2:14)***